

MWANGA MKUU UNAONG'AA

 Somo langu asubuhi ya leo linapatikana katika Agano Jipya. Kwanza kutakuweco na somo la Maandiko kutoka Mathayo 1 . . . sura ya 2, kuanzia na aya ya 1. Na tena pia nataka kuchukua, kama somo, kwenye sura ya 4, na aya ya 14 na ya 15. Napenda sana kusoma Neno, kwa maana Neno ni Mungu.

Yesu alipozaliwa katika Bethlehemu ya Uyahudi zamani za mfalme Herode, tazama, mamajusi wa mashariki walifika Yerusalemu, wakisema,

Yuko wapi Yeye aliyezaliwa Mfalme wa Wayahudi? Kwa maana tuliiona nyota yake mashariki, nasi tumekuja kumsujudia.

² Kisha katika sura ya 4 na aya ya 14, ikinena kuhusu yule nabii.

Ili litimie neno lililonenwa na nabii Isaya, akisema,

Nchi ya Zabuloni na nchi ya Naftali,

Njia ya Bahari, ng'ambo ya Yordani,

Galilaya ya mataifa,

Watu wale waliokaa katika giza

Wameona mwanga mkuu,

Nao waliokaa katika nchi ya uvuli wa mauti

Mwanga umewazukia.

³ Nataka kuchukua somo langu kutoka kwenye . . . kama hili: *Mwanga Mkuu Unaong'aa*. Ni Andiko lisilo la kawaida sana.

⁴ Kwenye, wakati kama huu, watu kwa kawaida wamehubiri sana juu ya “hamna nafasi katika nyumba ya wageni,” kwenye majira haya ya sikukuu ya Krismasi, na “Yusufu na Mariamu,” na—na “kuzaliwa kwa Bwana Yesu.” Jana nilikuwa nikifikiri ningejaribu kuliendea kwa njia tofauti, maana wengi wenu mnasikia kwa redio na televisheni.

⁵ Na nilipokuwa nikiwaza, hili lilikuja mawazoni mwangu, kuhusu wale mamajusi na ile nyota. Na lililonigusa lilikuwa, kwamba, mamajusi ana uhusiano gani na Kristo? Kwa hiyo, kwa kuwasoma wengi wa wanachuoni wa kale, jana usiku, usiku sana, mpaka nikalala kwenye dawati, nikijaribu kupata jambo fulani linaloweza kuleta mwanga kidogo juu ya somo la siku ya leo.

⁶ Basi, ni jambo lisilo la kawaida kuzungumza juu ya mambo haya, kwa sababu, hata hivyo, Mungu si wa kawaida. Mungu hutenda mambo kwa njia isiyo ya kawaida, na wakati mwingine katika wakati usio wa kawaida, kwa maana Yeye si wa kawaida

kabisa. Na wale wamtumikiao si wa kawaida; ni watu wa kipekee.

⁷ Kwa hiyo wakati sisi, wakati huu wa majira haya, tunapoyaelekeza mawazo yetu kwenye Krismasi, ni vibaya sana kwamba inatubidi kuiweka kwenye hadithi ya uongo inayoitwa “Baba Krismasi,” badala ya kuwa Krismasi halisi inayopaswa kuwa. Watoto wengi nchini leo hawajui zaidi ya eti Krismasi maana yake ni “gari la kuteleza barafuni lililojaa vitu vya kuchezea watoto, na kulungu wa fumbo akiivamia nyumba,” halafu baadaye wanakuta kwamba hadithi hii ni ya uongo; hata inatatiza imani yao, wanapofikia kuijua hadithi ya kweli ya Krismasi, ya kwamba haikuhusiana kamwe na kulungu, ama mtu anayevuta kiko, mwenye koti lenye sufu.

⁸ Ilikuwa ni kuzaliwa kwa Bwana wetu Yesu aliyebarikiwa. Na ni jambo lisilo la kawaida sana kuona jinsi Mungu alivyotenda kazi kwa njia hii, kwa sababu hakuna wakati mwingine ungalifaa katika historia yote ya ulimwengu. Ilipaswa iwe katika wakati huu hasa. Na sasa kwa muda mchache na tuangalie hayo majira.

⁹ Ilikuwa wakati ambapo Herode, yule muuaji, alipokuwa mfalme. Ilipaswa iwe, mtu huyu asiye na huruma alipaswa awe mfalme wakati huo, kwa maana tunayajua Maandiko yaliyosema “aliwaua watoto wote tangu umri wa miaka miwili kwenda chini,” akijaribu kumpata Kristo. Na ilipaswa iwe tu kwenye wakati huo.

¹⁰ Na pia kulipaswa kuwe, wakati huo, ilipaswa kuwe na kutozwa ushuru, kuwafanya Mariamu na Yusufu kurudi kwenye mji wa uenyeji wao wa Bethlehemu ambako walikuwa wamejiandikisha, na kuzaliwa kwao kulikuwa katika kumbukumbu ya behewa na katika hekalu, kutozwa ushuru. Naye Kristo alipaswa azaliwe Bethlehemu, nao walikuwa maili nyingi wakati jambo hili lilipotukia.

¹¹ Nasi tumejulishwa habari za hatari zilizowabidi kupitia, kusudi wafike kule. Sasa hawakuwa na gari zuri mno la kuwachukulia wagonjwa kumpandisha Mariamu kule. Nayo mambo hayakuwa kama yalivyo leo, kwamba tungekuwa na udhuru wa namna fulani. Ilikuwa amri ya mfalme. Hakuna kutoa udhuru. Lazima itimizwe. “Mfalme alisema hivyo!” Haidhuru alikuwa na hali gani, ama nini, hawana budi kurudi kwenye nchi ya uenyeji wao. Hakuna raha kwa maskini huyo mama mja mzito. Na hakuna njia ya usafiri; ni kwa miguu tu, ama juu ya punda.

¹² Nasi tunaambiwa ya kwamba Yusufu alimchukua Mariamu, mama huyu ambaye angejifungua wakati wo wote, akamweka juu ya punda mdogo. Na kama mtu ye yote ameshawahi kupanda punda, anajua jinsi ulivyo rafu mwendo huo. Maskini jamaa huyo, katika mkondo mrefu na mwembamba ambao unapindika

milimani, akija Bethlehemu, kutoka Yuda ya chini, barabara mbaya sana ya mawe-mawe. Vipi kama maskini punda huyo asingekuwa hodari wa kutembea, na angalianguka pamoja na maskini mama huyu mja mzito?

¹³ Ama, katika siku ambazo kulikuwa na usafiri mwingi sana watu wakienda kwenye nchi ya uenyeji wao, nchi nzima ilikuwa kwenye harakati ya kazi, imejaa wahaji na wasafiri, wakirudi kwenye nchi ya uenyeji wao, hali ambayo ni chombo kizuri sana kwa wanyang'anyi siku hizo. Walipoona misafara ya watu wachache; hao wapanda farasi, wanyang'anyi wangelipanda farasi wawaendee na kuwaua, na kuteka mali zao na kwenda zao. Lilikuwa jambo gumu jinsi gani kwa maskini huyu mume na mke, lililobidi kukabili, na jinsi lingalikuwa.

¹⁴ Pia, vipi kama baadhi ya wanyama wa mwituni, ambamo kulikuwa na simba wengi na wanyama wengi wa mwituni washambulizi, wanyama wakali ambao walizurura jangwa walizopaswa kuvuka. Vipi kama mnyama mkali angalilivamia hilo kundi dogo, Yusufu angalifanyaje na fimbo mkononi mwake, na mke ambaye ilikuwa vigumu kwake kutembea? Iliwalazimu kukabili hayo.

¹⁵ Bali inatupa faraja kujua jambo hili, kwamba sisi hatushikili kikomo cha maisha yetu. Mungu ndiye anayeshikilia kikomo cha maisha yetu. Naye ameamuru iwe hivyo, na hakuna kitu ambacho kitaukatiza mpango wa Mungu. Hatuna budi kuwasili.

¹⁶ Na hakukupaswa kuwepo na hofu. Na hata hivyo pengine Mariamu na Yusufu, wenyewe, watu wa kawaida tu, hawana elimu. Nao hawakuwa na njia ya kujua mambo haya, yaliyokuwa yakitendeka wakati huo, yalikuwa yakitimiza Maandiko.

¹⁷ Na ndivyo ilivyo leo. Mambo yanatendeka katika siku hizi tunazoishi, na wengi wetu hatuna habari nayo, jinsi Mungu anavyotenda kazi.

¹⁸ Niliulizwa hivi punde na mmoja wa hawa bibi wanaorekodi kwenye chumba hiki hapa, ni lini nitazungumzia juu ya somo hilo, la yale maandishi ya mkono, na sputiniki hewani. "Itakuwa Jumapili ijayo?"

Nikasema, "Sijui."

¹⁹ Lakini, loo, kuona wakati huu wa giza linalofunika, mkono mkuu wa Mungu unapiga hatua mbele taratibu. Hakuna kitakachoukomesha Huo.

²⁰ Na tunaweza kuona kama ilivyokuwa, leo, wakati hatimaye maskini yule punda pamoja na hao wasafiri wawili waliwasili. Walipokuwa wakija usiku, wanavuka jangwa, ilikuwa joto sana! Na basi hebu tuseme wanaketi juu ya mlima mdogo mashariki ya Bethlehemu.

²¹ Bethlehemu umo bondeni, na kuna mlima mdogo. Na barabara inayokuja Bethlehemu, inapinda mashariki ya Bethlehemu, kisha inatelemkia humo mjini. Karibu pembeni, mahali unapofanya mzunguko wa mwisho, kusudi uanze kutelemka hicho kilima, kuna lundo kubwa pale la miamba iliyochongoka. Na inadhaniwa na wanahistoria ya kwamba labda Mariamu na Yusufu walisimama pale wapate kupumzika kidogo kabla hawajashuka kwenda mji usiku ule.

²² Hebu tumtazame Yusufu, katika kutenda kwake kwa huruma, anamchukua na kumteremsha maskini bibi-arusi wake juu ya punda na kumweka chini, anamchukua na kumweka juu ya mwamba, kisha akasema, “Mpenzi, ule pale ule mji mdogo, chini yetu tu, ambao labda mgeni wetu mdogo atazaliwa.”

²³ Naweza kuwazia nikiona nyota zikimetameta na kuangaza tu kidogo, huku wao wamekaa wakiutazama Bethlehemu, kwenye ninino yao . . . mashariki yao. Nao walipokuwa wamekaa pale, huku wakiangalia nyota kwa mshangao; mbali sana, mamia ya maili mashariki ya mahali pale, kulikuwa na tamasha jingine lililokuwa linaendelea.

²⁴ Mnajua, Mungu hutenda kazi katika ulimwengu Wake. Anafanya mambo yatendeke katika nchi moja, huku anayaandaa yajitengeneze ili yatukie katika nyingine. Hapo tunaona, mbali sana kule mashariki, kama tunavyoambiwa na wanahistoria wengi, kwamba watu hawa, wale mamajusi, kama tunavyowajua walivyo.

²⁵ Leo hii wao wangukuwa, kwa njia moja au nyingine, wangeitwa, “wenye elimu ya nyota,” si kwa maana ya wapiga ramli; bali kuna elimu bandia ya nyota, ambayo inaitwa kupiga ramli. Na watu wanakimbilia mambo hayo, ambayo ni mawazo ya uongo ya elimu halisi ya nyota.

²⁶ Hampton alitwambia, yule mwanahistoria maarufu, ya kwamba ilikuwa . . . Wao walikuwa Wamedi-wa-Waajemi, hawa mamajusi. Hebu tuyafuatilie maisha yao kidogo. Na tunaona ya kwamba Wamedi-wa-Waajemi walijua Injili ya Bwana wetu walipokuwa huko Babeli. Miaka kadha kabla, katika wakati wa Mfalme Nebkadreza, walikuwa na watu kama mamajusi, ambao walizichunguza nyota na sayari za mbinguni. Nao wangalijua kwa ishara na kusogea kwa nyota, juu ya mambo ambayo yangetendeka.

²⁷ Na hao wafalme wa kale waliwataka shauri watu kama hao wapate kujua matukio na mambo ambayo yangetukia. Mungu daima huyatangaza hayo kwa sayari Zake za mbinguni kabla hajayatangaza duniani. Mungu huyaandika mbinguni.

²⁸ Na nyota ambayo sisi huangalia, na tunazifikiria kama vikundi vyenye ncha tano mbinguni, lakini, hizo ni, hizo ni dunia kubwa mno kuliko dunia hii, zikirudisha mng’ao wa jua.

²⁹ Na watu hawa bila shaka walipata kuifahamu Injili katika miaka ya uhamisho wa Israeli, wa miaka sabini katika nchi ya Wakaldayo, na, hakika, Danieli alifanywa mkuu wa hao mamajusi. Huyu nabii, kwa hekima yake kuu ya kujua mwisho wa mambo, na kujua ambayo Mungu angetenda, naye alitwa mkuu wa mamajusi. Nao hao mamajusi walikuwa na magombo ya kale waliyokuwa wakiyarejea, ya baba zao wa kale. Naye Danieli akaleta maandiko ya Bwana.

³⁰ Na kwa hiyo tunafahamu ya kwamba mnamo wakati huu wao walikuwa wameshauriana sana pamoja, nao walikuwa wameona hekima na nguvu ambazo yule Mungu mmoja na wa kweli alizotoa, ambazo zilikuwa za hali ya juu sana kuliko mwenye elimu ya nyota ye yote au mamajusi. Hiyo ilitibitishwa katika ule usiku wa Mfalme Nebkadreza...au ule wa dansi ya Belshaza, ya kwamba, hakuna hata mmoja wa Wakaldayo ama mamajusi angaliweza kuyasoma yale maandiko kwenye ukuta. Lakini Danieli, kwa Roho na nguvu za Mungu aliye hai, angaliweza kufanya hivyo. Na maandiko yake yaliwekwa wakfu, na ni wakfu hadi siku hii.

³¹ Sasa tunawaita, huko mashariki...Nimekuwa na majaliwa ya kuzungumza nao huko India. Nao sasa wanaitwa Waislamu. Bali kweli walikuwa Wamedi-wa-Waajemi. Wahindi wanaitwa...naamini wao wanawaita najisi. Nao Wamedi-wa-Waajemi kweli ni Waislamu. Nao ndio ambao hapo awali walikuwa na Mfalme Nebkadreza. Na wataalamu wao ndio wanachuoni waliosoma ma—mambo ya asili, wapate kutangaza mambo ya kiroho yatakayotukia.

³² Kwa hiyo katika muda huu mrefu wa miaka hii mia kadha, na magombo ya mafundisho ya Danieli, na kadhalika, waliyaweka.

³³ Basi walivyofanya, nyakati za mapema jioni, Wageenda kwenye Milima ya Assay[?]. Na mahali hapa walikuwa na ngome. Na katika ngome hii kulikuwa na ngome ya mamajusi. Nao wangepanya karamu yao ya fujadous[?]. Na baada ya hiyo karamu wangetembea kwenye paa la ngome, ama mahali palipoinuka, na pale kwenye mnara wa kuchunguzia baada ya jua kutua. Na kama ilivyo kawaida ya Waislamu, wanalisujudu jua na kupiga kelele, "Allah! Allah!" Na mara nyingi wanajibariki kwa maji matakatifu, na kadhalika, hata wa sasa. Mara nyingi, moja ya vifaa vyao vitakatifu sana, kilikuwa moto. Waliadini ya kwamba Mungu huyu mmoja aliye wa kweli aliishi katika moto.

³⁴ Na ni jambo la ajabu jinsi gani kujua ya kwamba huyu Mungu mmoja wa kweli na aliye hai kweli huishi katika Nuru, Naye ni Moto ulao.

³⁵ Jinsi ambavyo wao waliwasha mioto mitakatifu! Nao waliutazama moto huu, kwa maana waliadini ya kwamba yule

Mungu mmoja na wa kweli aliishi katika moto huu, naye alirudisha mng'ao Wake kwao. Nao huo moto uliwaka sana wakati—wakati nuru ya jua ilipotua.

³⁶ Na kwa hiyo wangepanda kwenye mnara huu wa kuchunguzia, nao wangeinua macho yao juu. Walikuwa wamefundishwa vizuri. Nao walijua kila msogeo wa kundi kuu la nyota za mbinguni. Walichunguza kwa makini wapate kuona msogeo wo wote.

³⁷ Loo, laiti Wakristo wangaliweza kufanya hivyo! Si kuzitazama nyota, bali kuliangalia Neno la Mungu likifunuliwa. Kama tu tungalitambua leo, na kuona jinsi Mungu ameahidi katika siku hii mambo ambayo tumeyashindania kwa ushujaa sana. Mungu ameahidi kufanya mambo haya, kama vile kuwaponya wagonjwa na kufanya miujiza mikuu.

³⁸ Danieli yule yule aliyewafundisha juu ya yale matukio, alisema, ya kwamba, “Katika siku za mwisho watu wanaomjua Mungu wao watafanya mambo makuu.” Maandiko hayo hayana budi kutimizwa. Laiti tungalichunguza! Na kama utachunguza, Mungu hujifunua tu kwa hao wamtafutao na wana hamu ya kumwona Yeye. “Nikaribieni Mimi, Nami nitawakaribia,” asema Bwana. Na wakati mwingine Mungu huacha mambo yatendeke ili kwamba tumkaribie Yeye. Kwa maana kweli Mungu ameamuru kwamba matukio fulani hayana budi kutukia, na yatajifunua wakati tu saa yake kuu inapowadia.

³⁹ Na katika, tutasema, usiku fulani, baada ya karamu kwisha, nao walikuwa wamekusujudia kutua kwa jua, kundi letu linapanda linaenda kwenye mnara huu wa kuchunguzia. Na wakati zile sayari kuu za mbinguni zilipoanza kuonekana mbinguni, magombo ya zamani za kale, ya wataalamu, yakatolewa. Kisha yakafunguliwa, nao wakayaangalia, wakasema, loo, mambo fulani yaliyotabiriwa. Na hayo mazungumzo, labda, yakaingilia mambo ya zamani za kale, juu ya kuanguka kukubwa kwa falme, na kuanguka kwa milki zao kubwa, na jinsi maisha ya jamii yalivyokuwa, na vita, ambavyo vilikuwa vimeivuruga nchi na kuilowesha kwa damu ya wenzi wao. Na kama vile watu walio wa kiroho hufahamu tu mambo ya kiroho; jinsi zile nyakati kuu zilizopita zilivyofunuliwa, na aibu zao, huku ule moto mtakatifu unawaka ukielekea juu kisha ukatoweka, kumwakilisha Mungu mmoja wa kweli na aliye hai.

⁴⁰ Na usiku ulivyoendelea hata ukafikia katikati, tuseme, saa nne ama saa tano, wakati jeshi hili lilipokuwa limeketi pale, labda likiimba nyimbo zao, ama labda walikuwa wanaomba. Hatujui hasa walichokuwa wakifanya, na hao wanahistoria hawakifanyi dhahiri. Bali, hata hivyo, hapana shaka walikuwa katika nia ya kiroho, kwa maana Mungu huabudu palipo na umoja na roho.

⁴¹ Mungu atatuja asubuhi ya leo. Atayaokoa maisha ya msichana huyu mdogo mpendwa, na wengi wenu hapa ambao labda wanakufa kwa kansa na magonjwa mengine, kama tunaweza tu kuwa katika umoja wa kiroho na Neno Lake pamoja Naye. Mungu atajifunua Mwenyewe. Yeye hufanya hivyo daima.

⁴² Huko njiani wakielekea Emau, baada ya kufufuka, ilikuwa tu wakati Theofilo na rafiki yake walianza kuzungumza Naye, na Maandiko yakanukuliwa, kisha Mungu katika Kristo akajifunua Mwenyewe kwao. Ndipo walipokuwa wakirudi, wakasema, “Je! mioyo yetu haikuwaka ndani yetu hapo tulipokuwa tukisema Naye njiani?” Kitu fulani kuhusu kuzungumza juu ya Neno!

⁴³ Na katika magombo yao ya kale, walipokuwa wanasoma juu ya mamajusi mbalimbali waliokwisha kufa. Nami siwezi kutamka Biblia yao wakati huu, ama waliita Zedakoah[?], kitu kama hicho, ambayo walisoma na kurejea kwenye maandiko haya ya watu wao watakatifu. Na jinsi ambavyo wengi wao walikuwa waabudu sanamu, na kuleta aibu na fedheha kwa watu, hapana shaka hawa mamajusi waliviinamisha vichwa vyao kwa aibu. Lakini, hata hivyo, moto matakatifu uliowaka, ulimwakilisha Mungu wa kweli.

⁴⁴ Ndipo naweza kuona mtu mmoja akija kutoka kwenye ile ngome, amebeba gombo mkononi mwake. Naye akawapa hao wataalamu huku wameketi kwenye ule mnara wa kuchunguzia, wakiziangalia nyota, na kila kitu kikiendelea katika upatanifu mkamilifu, kama zilivyofanya usiku baada ya usiku, kama tu Mungu alivyoziamuru.

⁴⁵ Na humu ndani, huku wanazungumzia juu ya kuanguka kwa falme, walisoma fungu moja la Danieli, ambalo lilisema, “Nami nikatazama hata jiwe likachongwa mlimani, bila kazi ya mikono, nalo likazipiga falme za duniani zikawa—zikawa makapi ya viwanja vya kupepetea. Nalo jiwe hili kuu likawa mlima mkubwa likaijaza dunia yote. Na ufalme Wake utakuwa ufalme wa milele.” Matumaini yao basi yalichochewa kufikia wakati ambapo milki zitaacha kuanguka, na wakati falme zitaacha kuangamizwa, kwa maana waja ufalme wa milele uliokusudiwa na yule Mungu mmoja wa kweli na aliye hai.

⁴⁶ Na walipokuwa wanawazia mambo haya, juu ya Maandiko, mmoja hapana budi aliinua macho yake. Na kulikuweco na mgeni kati yao. Wakaona Mwanga ambao hawajauona hapo kabla. Ilikuwa Nyota yenye fahari ambayo haijapata, mpaka wakati huu, kuwemo, ama haijaonekana kwa macho ya yule mamajusi. Bali ilikuwa hapo. Kwa nini? Maandiko hayana budi kutimizwa.

⁴⁷ Mnasema, basi, “Ndugu Branham, unafikiri Mungu angejishughulisha na hao mamajusi?”

48 Biblia ilisema, katika Waebrania sura ya 1 na aya ya 1, ya kwamba, “Mungu, kwa sehemu nyingi na kwa njia nyingi,” kwa njia za kila namna, “alisema na baba zetu.”

49 Imeandikwa pia katika Matendo 10:35, ya kwamba, “Mungu hana upendeleo, bali Yeye huwaheshimu wale, katika kila taifa, wanaotamani kumtumikia katika haki.” Ingawa waweza uwe katika kosa, hata hivyo, katika haki ya—ya mwelekeo wa moyo wako kwamba unataka kumtumikia Mungu, Mungu ataheshimu jambo hilo. Kwa hiyo, basi, madhehebu hawana mipaka wanayoweza kuweka, ambayo itamkomesha Mungu kwenye kanuni yo yote ya imani, kwa maana Mungu ataangalia kusudi la moyo wa binadamu, na hapo atafanya kazi kuanzia mahali hapo.

50 Nasi tunaona ya kwamba hawa mamajusi, wakiwa waaminifu mioyoni mwao na wakitaka kumwona huyo Mungu mmoja na wa kweli, na wakitazamia unabii Wake utimizwe, ambao ulisema ya kwamba, “Bwana atamwinua Yeye na kufanya... Ufalme Wake hautakuwa na mwisho. Utakuwa ufalme wa milele.”

51 Ilikuwa ni wakati huo ambapo ile Nyota, tunayojua leo inaitwa Nyota, ilitokea mbinguni. Naweza kuwazia hao mamajusi, kwa moyo mmoja, walisimama kimya kwa mshangao huku wakiangalia lile tukio la ajabu la Nyota ambayo ilikuwa imeasi kanuni za mfumo wa jua, nayo ilikuwa imetoka kwenye lile kundi kubwa la sayari za mbinguni, kutangaza jambo fulani wakati lilipokuwa karibu kutukia.

52 Natumaini kufikia wakati huu mnaweza kusoma katikati ya mistari na kujua tunalomaanisha, ya kwamba katika siku hii, Mungu ameasi kila kitu, kujitangaza Mwenyewe, ya kwamba Yeye yu hai leo, amefufuka kutoka kwa wafu, katika Mwili Wake mkuu wa mbinguni. Picha hii hapa ya Utu Wake ingemwasi kila kafiri ulimwenguni. Yu hai milele. Mungu hutenda mambo katika njia Yake Mwenyewe, isiyo ya kawaida.

53 Lakini, walikuwa wamechunguza ile mianga ya mbinguni, lakini Mwanga huu ulionekana tofauti na mingine yote.

54 Nasi tumechunguza, leo, mianga kanisani. Tumechunguza mianga ya Kimethodisti, Kibatisti, Kipentekoste, Kipresbiteri.

55 Bali kwa hao wanaomtazamia, yaonekana kuna Mwanga tofauti ambao umeanza kuangaza, ambao unamtangaza Yeye. “Ni yeye yule jana, leo, na hata milele.” Katika uzuri Wake mkuu na wenye fahari pamoja na nguvu Zake, wa ule Mwili wa mbinguni ambao umetumwa katika umbo la Roho Mtakatifu, katika siku hizi za mwisho kwa Kanisa, kuutangaza uweza wa kufufuka Kwake, na Yeye daima ni Mwanga wa Milele ambao sasa unaishi miongoni mwa Waamini Wake. Loo, ni ajabu jinsi gani kuona yale afanyayo!

⁵⁶ Na hapo huku wamesimama, wameduwaa, mmoja hangalimzungumzia mwingine, kwa maana utukufu wa Mwanga huu uliwaduwa.

⁵⁷ Loo, jinsi ilivyo leo, rafiki yangu mdhaifu, kwamba wakati mtu ambaye hajajua Nguvu Zake, kutoa Mwanga mpya na kutoa tumaini jipya, wakati anapotembea na kuingia katika Uwepo wa Utu wa Kiungu wa Kristo, kwa imani inayomfanya aduwae kwa ajili ya utukufu Wake. Si kama vile unaenda madhabahuni na kumpa mhudumu mkono wako wa kuume, wala si kama kwenda kwenye kidimbwi kubatizwa, ama kusimama na bakuli ukanyunyiziwe. Ni kutembea ukaingia katika Mwanga ambao hujapata kuuona hapo awali. Ni nanga ya imani ya Kiungu ambayo huita cho chote kinyume cha Neno la Mungu kama kwamba hakikuwapo. Inaweka Uhai mpya. Inawapa tumaini wanaokufa. Inawapa moyo walio wanyonge. Inawapa uponyi walio wagonjwa. Inawapa baraka hao wasiopendwa. Ni ajabu jinsi gani kuingia katika Mwanga wa Uwepo Wake! Si hadithi ya kubuniwa. Wala si kitu ambacho mtu fulani, bongoni mwake, amepanga kimwili. Bali, ni kuja moja kwa moja katika Uwepo wa Mfalme wa Utukufu, Nuru ya Milele ya Mungu aliye hai.

⁵⁸ Wakati jambo fulani linapotukia, hilo hutia nanga hilo tumaini ndani yako, kwamba haidhuru u mgonjwa jinsi gani, baadaye, haimfai Ibilisi kitu kuthubutu kukujaribu kwa lo lote ambalo ni kinyume chake. Umetia nanga milele. Haidhuru huyo adui atakufanya ujaribu kuishi maisha mabaya jinsi gani, umetiwa nanga milele, kwa maana umeingia katika Uwepo Wake, ukaingia katika Mwanga wa Kiungu ambao umeshabadilisha utu wako wa ndani na kuweka furaha, kengele ya wokovu, ikilia moyoni mwako, ambayo ulimwengu haujui kitu juu yake, ya kwamba umepita toka mautini ukaingia Uzimani. Mauti na vivuli vyake vimekutoroka, na umekuwa kiumbe kipya unapoingia katika Mwanga huu wa Kiungu.

⁵⁹ Hao mamajusi waliposimama, wameduwaa, walipokuwa wanautazama Mwanga huo, mwishowe naweza kusikia mmoja akimwambia mwenziwe, "Loo, hii si ni ishara ya ajabu kwamba jambo fulani liko karibu kutukia!"

⁶⁰ Kweli, leo, pia, tunapokuja katika Uwepo wa Bwana Yesu, ni ishara ya Kiungu kwamba jambo fulani liko karibu kutukia; Kuja Kwake kwa pili kwenye fahari kumekaribia.

⁶¹ Basi walipoangaliana, mmoja kwa mwingine, na baada ya kitambo kidogo... Waliuangalia, labda, usiku kucha. Jinsi ulivyong'aa! Ulionekana mwangavu kuliko nyota zingine. Ilionekana kama kwamba hawangeweza kuyaondoa macho yao Kwake, kuiangalia nyota nyingine yo yote.

⁶² Nami nina hakika, kama tukiua huo Mwanga wa Milele ukiangazia nyuso zetu, hatutayaangalia madhehebu yetu, kusema, "Sisi ni Wabatisti, ama ni Wapresbiteri, ama ni

Wapentekoste,” ama yo yote yale. Tunaangalia tu kwenye ule Mwanga, na kuishi. Yeye ndiye Mwanga wa Milele.

⁶³ Nao walipokuwa wanautazama Huo, wakati jua hatimaye lilipochomoza. . . Wao hulala mchana. Nimewaona wameketi barabarani huko India, wameikunja miguu yao, wakaunganisha vichwa vyao; kwa kuwa wao wanalala mchana, na usiku wanaondoka wanaenda kuchunguza nyota, wakichunguza kwa makini msogeo wo wote.

⁶⁴ Ni wale tu wanaomtazamia watakaomwona Yeye. Ni wale tu wanaomwamini watakaofurahia baraka Zake. Ni wale tu wanaoamini kuponya watakaopokea uponyi. Ni wale tu wanaoamini wakovu watakaoupokea. Mambo yote yawezekana kwa hao waaminio. Lakini, kwanza, lazima isiwe tu wazo lililowaziwa kimwili. Lazima iwe ni ufunuo wa moja kwa moja uliotumwa kutoka kwa Mungu peke yake, huku tunaangalia.

⁶⁵ Tunaona, usiku baada ya usiku, wao walivangalia. Wakazungumzia habari Zake. Waliyaangalia Maandiko, na katika kuchunguza. Naweza kumwona mmoja akija, na kusema, “Hapa kuna Maandiko mengine ya Kiebrania. Yanatoka kwa mmoja wa manabii wao, jina lake Baalamu. Naye alisema, “Nyota itainuka kwa Yakobo.” Nao wakayaona Maandiko yakitimizwa. Loo, jinsi mioyo yao ilivyofurahi!

⁶⁶ Na jinsi ingepaswa kuifanya mioyo yetu kufurahi, kujua ya kwamba katika nyakati hizi mbovu tunazoishi, kuona Maandiko matakatiifu ya Mungu yakitimizwa na kufunuliwa kwetu kama Mwanga mkuu unaochunguza juu ya utu wetu.

⁶⁷ Halafu, baada ya kitambo kidogo, walipokuwa wakiutazama, ajabu ni kwamba usiku mmoja ukaanza kusogea. Nasi daima tunasogea pamoja na Mwanga. Basi huo Mwanga ukaanza kusogea kuelekea magharibi. Upesi wakatayarisha ngamia wao na mali zao zote. Wakachukua zawadi. Nami naweza kuwaona wanapoanza safari yao, wakiufuata huo Mwanga, kwa maana wao walijua kilikuwa Kiumbe cha kimbinguni. Kilipaswa kurudisha mng’ao wa Mwanga fulani mkuu zaidi.

⁶⁸ Ndivyo ilivyo leo, rafiki, tunapoona nyota ikiangaza, tunajua ya kwamba ni kurudisha mng’ao wa jua. Tunapouona mwezi ukiangaza, tunajua huko ni kurudishwa kwa mng’ao wa mwanga mkuu zaidi.

⁶⁹ Tunapoona kanisa likiangaza, tunajua ni kurudishwa kwa mng’ao wa Mwanga mkuu zaidi, ule Mwanga usiozimika na wa Milele. Bali wakati tunajitia giza, na kuigeuza mioyo yetu, na kuiondoa imani yetu, na kusema, “Siku za miujiza zimepita, na hakuna mambo kama haya tena,” tunaupa kisogo Mwanga wa Mungu wa Milele.

⁷⁰ Na walipokuwa wanasonga mbele, naweza kuwaona wakiondoka milimani wanaenda kwenye mitelemko ya

magharibi. Waliifuata hiyo mitelemko hata kwenye Mto Tigris, na hapo wakaufuata huo mto mkuu Tigris hata wakaingia Babeli, wakavuka kivuko kwenye Frati, wakashuka wakaenda, wakaizunguka nchi ya Palestina. Huku wakifurahi! Wao walisafiri usiku kwa maana ilikuwa baridi kidogo wakati wa usiku, kwa wao kuisafiri kupitia jangwani. Jambo lingine lilikuwa, nyota ziliangaza usiku, kwa hiyo iliwabidi kuufuata ule Mwanga. Na huo Mwanga ulikuwa kiongozi wao.

⁷¹ Nao walipokuwa wanakuja, hatimaye ukafika Yerusalemu. Lakini, Huo ulipofika Yerusalemu, ukazimika. Mara ukatoweka walipofika Yerusalemu, kwa maana huo ulikuwa wakati wao basi kuuangaza huo Mwanga.

⁷² Basi wakashuka wakaenda kupitia barabara zilizopindapinda za jiji hilo mashuhuri, wakashuka wakaenda kupitia barabara za huo mji mkuu wa kale wa dunia, ulio karibu mkuu, Yerusalemu; uliokuwa makao makuu wakati mmoja ya yule Melkisedeki mkuu, ambao manabii wakuu wa kale na waandishi waliandika habari zake. Bali katika maisha yao ya kivivu, ya kimwili, yaliyopumbazwa nusu na yasiomcha Mungu, hiyo Nuru ya Injili ilikuwa imezimika.

⁷³ Na hawa hapa watu wa Mataifa, katika mji wa Wayahudi, wakipaza sauti, “Yuko wapi Yeye aliyezaliwa Mfalme wa Wayahudi? Kwa maana tumeona nyota Yake mashariki nasi tumekuja kumsujudia.” Ni tukio la ajabu jinsi gani la siku hii. Ee Baba wa rehema, tunapoangalia na kuwazia! Wayahudi walilala sana hata mamajusi, Wamataifa wa mashariki, walikuja kutoka nchi za mbali, wakisafiri kumtafuta Mfalme wa Wayahudi, nao hawakujua neno juu yake.

⁷⁴ Leo, Mungu amewachukua wanaume wasio na elimu, wavulana kwa wasichana ambao labda hawana elimu zaidi ya sekondari, akawainua kwa nguvu za Roho Mtakatifu, wanaopaza sauti katika masikio ya kanisa, “Yeye yuko hapa katika nguvu Zake kuu, apate kujifunua Mwenyewe na kujijulisha,” na kanisa halijui neno juu yake.

⁷⁵ Wao walikuja kumsujudu. Walikuja kutoa heshima zao kwa Mfalme wa wafalme. Nalo kanisa, katika usingizi wao wa kimadhehebu, halijui kitu juu Yake. Wao ni wageni. Vipi, wakati hawa wanyama waliochangamka, huku wamevikwa vitambaa maridadi vya kimashariki, vikining’inia pande zote, na vishada. Na kama Philon alivyosema wakati mmoja, “Hawakuwa wafalme, bali walikuwa—walikuwa mashuhuri vya kutosha kuwa wageni wa heshima wa yule Mfalme.” Na hawa hapa wameketi juu ya hawa wanyama wenye fahari, huku wanatembea barabarani, wakisema, “Yuko wapi Yeye aliyezaliwa Mfalme wa Wayahudi?” Biblia ilisema ya kwamba, “Herode alifadhaika na Yerusalemu pia pamoja naye.” Ushuhuda wao ulichochea kitu fulani.

⁷⁶ Si ni vibaya sana leo, ya kwamba kanisa haliwezi kuinuka likatoka katika upumbavu wake wa mazoea ya kitheolojia, kuona nguvu za Kristo aliyefufuka na aliye hai, na za Utukufu Wake; huku mwenendo wa watu wa madhehebu yote watu wasiojua kusoma na wasio na elimu, unasambaa ulimwenguni! Njoni muone Utukufu wa Mungu aliye hai. Roho Mtakatifu anashuka tu kama alivyofanya hapo mwanzo. Maandiko hayana budi kutimizwa, na haya hapa katika wakati wa mwisho.

⁷⁷ Na wakati hawa mamajusi walipokuwa wanapita barabarani, walitaharukisha kuanzia mfalme hadi bawabu, kwa ujumbe, “Yuko wapi? Yuko wapi?” Hawakuwa na jibu. [Ndugu Branham anapiga makofi mara mbili—Mh.]

⁷⁸ Na, leo, wakati sputiniki zimejaa angani, wakati ishara za maangamizi ya kila kitu zimekaribia; wakati wanaume kwa wanawake wanajifurahisha katika dhambi na kuishi katika kutokumcha Mungu, watu wanapiga makelele, “Hii ina maana gani?” na kanisa halina jibu. Limelala usingizi.

⁷⁹ Lakini Roho Mtakatifu, Mwanga wa Mungu Usiozimika na wa Milele uko hapa kumwangazia mtu ye yote atakaye na anayeweza kuupokea Huo.

⁸⁰ Mwanga ulikuwa umeondoka. Walikuwa wakitoa ushuhuda wao. Na hatimaye wakaliita Baraza la Wazee likutanike, lifanye mkutano wa halmashauri. Nao wenye wataalamu na manabii wakaja, wakiwa na nabii mdogo, maskini nabii mdogo, jina lake Mikaya, unabii wake. Nao wakamwam’Ewemfalme, “Imeandikwa, ‘Ewe Bethlehemu, si wewe ndiwe mdogo sana miongoni mwa majumbe wa Yuda? Bali kwako atataka mtawala atakayewachunga watu Wangu, Israeli.’ Kwa hiyo haina budi kuwa Bethlehemu ndiko atakakozaliwa Kristo, Mfalme wa Wayahudi.”

⁸¹ Vema, hakuna mtu angaliwaambia jinsi ya kwenda Bethlehemu. Bali walitoka nje ya lango, na, wakati walipotoka katika huo mji wa giza, ule Mwanga ukaonekana mbele yao tena. Ile Nyota ikatokea. Na Biblia ilisema, “Walifurahi furaha kubwa mno.” Lazima kweli walipiga kelele kidogo. Walifurahi furaha kubwa mno. Walifurikwa na furaha. Wao...Nyota ilionekana kusudi iwaongoze hadi kwenye mwisho wa safari yao.

⁸² Wao wakaifuata. Ndipo wakaona ya kwamba ilining’inia chini kidogo kuliko ilivyokuwa. Iko karibu kidogo tu sasa. Na hatimaye...Wakaenda zao, wakifurahi na kumsifu Mungu, usiku kucha, wakiongozwa na mkono wa Bwana. Lakini hatimaye ile nyota ikaja kwenye hori ndogo, ambapo palikuwa mahali padogo kando ya kilima, pango, na hapo ile Nyota ikatua juu ya pango. Na hawa mamajusi wakuu sana, wamechukua zaidi ya mwaka mmoja na miezi sita katika safari yao, njiani, wakisafiri, wakiangalia, bila kufuata kitu kingine upande mwingine ila ile Nyota. Na wakati ilipotulia, wakaingia na mle

ndani wakamwona yule mtoto mchanga, Yusufu na Mariamu. Nao wakaleta zawadi kutoka katika sanduku lao la hazina. Wakampa Yeye, dhahabu, uvumba na manemane.

Laiti tungalikuwa na wakati! Hebu tusimame kwa dakika moja.

⁸³ Dhahabu iliwakilisha nini? Yeye alikuwa Mfalme. Hakuwa afanywe Mfalme; Yeye alizaliwa akiwa Mfalme. Yeye alikuwa Mfalme wa Milele wa Mungu. Alikuwa Mfalme, kwa hiyo wakampa dhahabu.

⁸⁴ Kisha wakampa uvumba. Hayo ni manukato, ghali mno, ndiyo bora sana ungaliweza kupata. Maana ya uvumba ilikuwa nini, hayo manukato? Yeye alikuwa harufu nzuri ya manukato kwa Mungu, kwa maana alienda kila mahali akiwaponya wagonjwa na kutenda mema. Dhahabu, kwa maana alikuwa Mfalme. Uvumba, kwa maana alikuwa harufu nzuri ya manukato kwa Mungu. Maisha Yake yalimfurahisha Yeye sana, hata Mungu akampulizia utakatifu Wake na uzuri, kwa maana ulikuwa ni utakatifu Wake Mwenyewe uking'aa katika Yeye.

⁸⁵ Loo, laiti tungalikuwa harufu nzuri ya manukato, laiti utakatifu wa Mungu ungalidhihirishwa ndani yetu; mpaka tungeenda kila mahali tukitenda mema, kama Yesu wa Nazareti, mpaka ingekuwa ni harufu nzuri ya manukato kwa Bwana.

⁸⁶ Lakini, tunagombana, tunabishana, tunazozana, tunaona shaka, hiyo ndiyo sababu inanuka vibaya puani katika mianzi ya pua ya Mungu. Maisha yetu yalikuwa yanaingia na kutoka mahali pa kale ambapo hatupaswi kuwemo. Tunasema mambo ambayo hatupaswi kuyasema. Tunafanya mambo ambayo hatupaswi kufanya. Tunabishana na kuungana na ulimwengu, na kumkana Kristo katika nyakati zilizo muhimu sana. Hiyo ndiyo sababu hatuwezi kuwa harufu nzuri ya manukato.

Lakini, Yeye alikuwa hivyo, na hawa mamajusi wakampa uvumba.

⁸⁷ Sasa wao walimpa manemane, pia. Na kila mtu anajua manemane ni mboga ghali sana na zenye uchungu. Manemane, manemane iliwakilisha nini? Ni dhabihu kuu mno. Maisha Yake machanga, yaliyopondapondwa pale Kalvari, ambapo dhambi za ulimwengu zilimsaga vipande vipande. Dhahabu, kwa sababu alikuwa Mfalme. Uvumba, kwa ajili ya maisha Yake mazuri na yenye kupenda. Na manemane, kwa sababu ya dhabihu Yake kwa ajili ya wenye dhambi, ndiyo sababu alikufa. "Hapo Yeye alijeruhiwa kwa makosa yetu, akachubuliwa kwa maovu yetu. Adhabu ya amani yetu ilikuwa juu Yake, na kwa kupigwa Kwake sisi tuliponywa." Hiyo ndiyo sababu walimpa manemane.

⁸⁸ Nao wakiisha kuonywa na Mungu katika ndoto, wakaenda zao kwa njia nyingine. Hawakurudi, bali safari ya—yao ilikuwa imekwisha. Ile Nyota ilikuwa imemaliza mwendo Wake.

⁸⁹ Ile Nyota ina maana gani kwetu, leo, ewe rafiki? Danieli anatupa jawabu, Danieli 12:3. Ilisema, “Walio na hekima na wanaomjua Mungu wao watang’aa kama mwangaza wa mbinguni; na hao waongozao wengi kutenda haki watang’aa kama nyota milele na milele.”

⁹⁰ Sisi tu nini, leo, basi? Sisi ni nyota. Kila Mkristo aliyezaliwa mara ya pili ni ushuhuda kwa Bwana Yesu Kristo, nyota ya kurudisha mng’ao wa nguvu na utakatifu wa Bwana Yesu; kumdhihirisha katika maisha Yake, kumkamilisha katika mazungumzo Yake, kumkamilisha katika nguvu Zake za Kuponya, kumkamilisha katika ufufuo Wake, kumdhihirisha Yeye katika kila njia aliyodhihirishwa na Mungu Baba. Sisi ni nyota.

⁹¹ Tazama! Inakupasa kuwa nyota ya aina gani? Nyota hii haikuongozwa na nguvu Zake Yenyewe. Iliongozwa na nguvu za kimbinguni za Mwenyezi Mungu. Na iwapo tutawadhihirisha wenye dhambi kwa Kristo, hatuna budi kuongozwa na Roho Mtakatifu. Warumi 8:1, ilisema, “Sasa, basi, hakuna hukumu ya adhabu juu yao walio katika Kristo, wasioenenda kwa kufuata mambo ya mwili bali mambo ya Roho.” Iwapo tutakuwa nyota, kurudisha mwangaza wa Kristo, kuwaleta wenye dhambi Kwake, hatuna budi kuongozwa na Roho Mtakatifu. Sawa!

⁹² Na hatuwezi kuwa wa kawaida. Hatuna budi kuwa wasio wa kawaida. Hatuwezi kuwa wa kawida, kwa sababu watu wa Mungu ni watu wa kipekee. Wamekuwa hivyo, katika nyakati zote.

⁹³ Ingawa ya kipekee, hata hivyo ile nyota ilikuwa na mwangaza mkubwa. Si kuangaza katika elimu ya kilimwengu, mambo ya ulimwengu, bali ikiangaza kama dhabihu mbele za Bwana. Tunasujudia, kama wale mamaajusi walivyofanya mbele za Mfalme wa wafalme, kurudisha mng’ao wa Mwangaza Wake.

⁹⁴ Wewe u nyota. Kila Mkristo ni nyota, kuwaongoza waliopotea, kuwaongoza waliochoka, mguu wa msafiri, kwa wale wanaotafuta. Pia, nyota haiwezi kujiongoza, haina budi kuongozwa na Roho. Haina budi kurudisha mng’ao wa Mungu maishani mwake, kuyaacha mambo ya ulimwengu, na kuishi kwa kiasi na utauwa katika maisha haya ya sasa. Haina budi kurudisha mng’ao wa Yule mkuu ambaye aliangaza.

⁹⁵ Tutafanyaje basi? Kuinuka, na kuangaza Mwangaza wa Mungu kwa wanaokufa. Katika kilindi cha giza la ulimwengu huu, inatubidi kurudisha mng’ao na kuangaza Uwepo wa Bwana Yesu katika uweza wa kufufuka Kwake. Kama alivyo jana, ndivyo alivyo leo, kurudisha mng’ao Wake.

⁹⁶ Lakini kumbuka, basi, ile Nyota, tena, ilipomaliza zamu yake, haitwai heshima yo yote. Ile Nyota iliwaleta tu wale watu mahali walikokuwa wakienda, na kuwaonyesha ule Mwangaza mkamilifu.

⁹⁷ Na sisi, kama washiriki wa Mwili wa Kristo, asubuhi ya leo, marafiki, sisi ni mianga ya Mungu, bali hatujitwali heshima sisi wenyewe. Tunapokuwa na mgonjwa we—wetu, we—wetu... mtu ambaye tunamwongoza; tunapokuwa nao, hatuna budi kutojitukuza na kuwaongoza kwenye “Mwanga mkuu na mkamilifu unaoangaza, kuangazia njia ya kila mtu ajaye ulimwenguni,” Bwana Yesu Kristo. Si hadithi ya kubuniwa inayoitwa Baba Krismasi, si kanisa la kimadhehebu; bali ule Mwanga wa kweli na ulio mkamilifu, Yesu Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai.

Na tuombe.

⁹⁸ Huku vichwa vimeinamishwa vikielekea kwenye mavumbi ambako Mungu alikutoa; siku moja, kwa uhakika kama vile nyota zinavyoangaza usiku, na jua kuangaza mchana, mtarudi mavumbini. Kama utakuwa hapa, kwenye mkeshwa wa Krismasi hii, na ungetaka Roho Mtakatifu akuongoze kwa Mwokozi, na unamkubali kwa njia hiyo, tafadhali mwinulie mkono na kusema, “Mungu, nirehemu. Ilangazie njia yangu ninapotembea kila siku. Na uniongoze, hatimaye, kwenye hiyo Nuru kamilifu, ili maisha yangu yaweze kupatananishwa na Yake nami nitapata Mwanga usiozimika na wa Milele.”

⁹⁹ Bwana akubariki, dada yangu mpendwa; nawe, dada yangu; nawe, ndugu yangu; wewe nyuma kule, ndugu; nawe, dada; nawe, ndugu yangu. Mungu anaona mikono yenu. Loo, wewe dada, Bwana anakuona. Naam, wewe hapa, bibi, Bwana anakuona, bila shaka.

¹⁰⁰ “Ee Yesu, mtume Roho Mtakatifu asubuhi ya leo, yaongoze maisha yangu yaliyopotoshwa. Nimekimbia na kujiunga na kanisa moja; nilikuwa Mkatoliki, kisha nikawa Mbatisti, kisha nikawa Mpresbiteri. Nilihudhuria la Kipentekoste. Nimeenda kila mahali. Nami nimekwisha tambua, Bwana, na—natangatanga tu; sijui ninakosimama. Bali jalia ule Mwili wa kimbinguni, jalia Kiumbe hicho cha kimbinguni cha ile Nyota ya Asubuhi, yule Roho mkuu wa Mungu, aniongoze leo kufikia mahali pale katika Yeye ambapo nataka kuwa, ambapo naweza kuweka moyo wangu horini na kumlea Huyu; ili Yeye apate kuniongoza kupitia vivuli vyote, mabonde ya vivuli vya mauti, kusudi nisiogope kitu nitakaposhuka kuja kwenye barabara hiyo.”

¹⁰¹ Kwaweza kuwa na mwingine kabla tu hatujafunga? Mungu akubariki, bwana; nawe, bwana; nawe, bwana. Naam, huo ulikuwa wakati mkuu wa wanaume, bwana. Huo mwingine karibu wote walikuwa wanawake; wakati huu wanaume ndio walioinua mikono yao. Hakika, ni watu wenye hekima ndio waliokuja, wakitafuta, wakiufuata ule Mwanga. Mungu anakutaka wewe. Maskini Mar-...

¹⁰² Maskini Mariamu na Yusufu walikuwa wameingia mjini, na hapo Yesu akazaliwa. Wakati wale mamajusi walipofika, walikuwa wamesafiri kwa muda mrefu, bali mwishowe walikuwa wamefikia kilele chao kikuu, ile Nyota ilikuwa imewaongoza. Sasa umekuwa ukitaka kuwa Mkristo kwa muda mrefu, labda umekuwa na safari ndefu. Hiki ndicho kilele asubuhi hii, labda, kwa maana sasa utampokea Yeye kama Mwokozi wako huku ukimlea moyoni mwako. Kuna mmoja zaidi, kabla hatujafunga mwito huu wa madhabahuni? Bwana awabariki. Vizuri sana. Asanteni.

¹⁰³ Na sasa ni wangapi wangesema humu ndani, “Ee Bwana, kama nilivyoambiwa na Maandiko, ambayo hayawezi kushindwa, ya kwamba katika manemanema haya uliyopewa Wewe, uliwakilishwa mle, ku’Wewewa kwa maisha Yako. ‘Wewe ulijeruhiwa kwa makosa yetu, kwa mapigo Yako tuliponywa. Wewe ulipigwa mijeledi yenye uchungu kwenye nguzo ya kupigia mijeledi, kusudi kupigwa Kwako kutuponye. Nahitaji nguvu Zako za kuponya, leo, Bwana. Naomba uondoe maishani mwangu mashaka yote. Yaondoe kwangu, nisije nikatilia shaka tena. Nijalie nije Kwako kwa unyenyekevu, sasa hivi, na nikuamini kwa ajili ya kuponywa kwangu.”

¹⁰⁴ Mwaweza kuinua mikono yenu, hivyo, ninyi wagonjwa? Bwana na akujalie mahitaji yako, rafiki yangu mpendwa.

¹⁰⁵ Mngeweza kumshuku Yeye? La hashu. Yeye anasimama leo kama yule Mwana wa Pasaka ama . . . kama Mwa—Mwana wa Krismasi, Mwana wa Mungu, Yule atoshelezaye kwa yote. Yeye hutimiza kila haja. Hutimiza kila haja uliyo nayo. Mpokee tu. Tumeambiwa tufanye nini katika Biblia? “Wekeeleni wagonjwa mikono nao watapata afya.”

¹⁰⁶ Sasa, Baba wa Mbinguni, nakuletea kundi hili dogo la watu ambao umewatuma asubuhi ya leo kusikia Ujumbe wa Nyota. Jinsi Wewe unavyowashughulikia watu wa kila tabaka! Unamshughulikia mwuza chang’aa. Unamshughulikia mlevi. Unamshughulikia mwanasayansi. Unamshughulikia mke nyumbani. Unamshughulikia mhudumu. Unamshughulikia mshiriki wa kanisa. Wewe ni Mungu. Wewe ni mkuu sana hata hakuna anayeweza kukutoroka. Na wale walio wanyofu mioyoni mwao, unawapa rehema hao wote wa mataifa yote na imani zote.

¹⁰⁷ Kwa hiyo tunakushukuru Wewe asubuhi ya leo kwa ajili ya wale walioinua mikono yao, yapata ishirini ama thelathini, ningekadiria. Nami naomba, Mungu, ya kwamba wakati uu huu, sasa hivi, ya kwamba ule Mwanga mkuu wa Milele utapenya uingie nafsini mwao, kusudi wapate ile amani ya moyoni ambayo wametamani na kuitafuta, kwa kujiunga na makanisa na—na kupitia taratibu fulani. Bali jalia Roho Mtakatifu awaangazie.

¹⁰⁸ Kama alivyosema Isaya, “Watu hawa walikaa katika giza kuu, Mwanga mkuu ukawaangazia.” Jalia, Bwana, ya kwamba hapo unabii huu upate kutimizwa leo katika mioyo hii ya hao wanaokutafuta. Wape hiyo amani ipitayo ufahamu wote, na iwapayo ridhaa kamilifu ya kwamba wamekutana Nawe na wamezungumza Nawe, na wakakutolea maisha yao, yaliyovunjika kabisa na kuraruliwa; ili kwamba Wewe, na dhahabu Yako, uvumba na manemane, upate kuwaponya na kuwafanya hao watu, vyombo vya heshima kwa ajili ya utukufu Wako. Tujalie, Bwana.

¹⁰⁹ Na sasa kwa wagonjwa na wanaoteseka, kuna utaratibu ambao Wewe umetupa, ya kwamba tunapaswa kuomba na kuwawekelea mikono. Nawe ulisema, maneno ya mwisho yaliyotoka katika kinywa Chako cha thamani, “Enendeni ulimwangu mwife mkaihubiri Injili. Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio; na wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya.”

¹¹⁰ Tunamjua mmoja, maskini mtoto mdogo mpendwa aliyelala hapa, ambaye amesafirishwa kwa ndege na watu waaminifu na wapendwa kutoka Florida, naye ni mahututi sana hivi sasa. Wakati, wengi wa watumishi Wako wameomba. Na—na madaktari wengi wamemwangalia na kutikisa vichwa vyao, wakasema, “Hakuna lingine.” Lakini ninashukuru sana kwamba maskini mama yule, na hao wanaohusika, hawako tayari kuchukua hilo kama jibu. Wameazimia kuona ya kwamba kila jiwe limepinduliwa. Kama tu wanaweza kupata kibali cha Mungu aliye hai, maskini kipenzi chao kitapata afya, na kitaishi. Loo, lijalie, Bwana, pamoja na wengine wanaoketi hapa.

¹¹¹ Wengi wameketi hapa asubuhi ya leo, ambao wangeweza kuinuka na kutoa ushuhuda kama wale mamaaji walivyofanya, “Tumeiona nyota Yake mashariki.” Wengi wangeinuka na kusema, “Tumeonja wema Wake, na tumehisi nguvu za kuponya Kwake,” ambazo zimetoa miilini mwao, kansa, na macho yaliyopofuka, na viungo vilivyolemaa, na magonjwa ya kila namna. Nasi tunatoa sifa Zake kwa sauti kuu, kwa sauti zetu zote, kwa mataifa yote, Bwana.

¹¹² Jalia hawa, asubuhi ya leo, watoto Wako walioko hapa sasa, wawe pia washiriki wa baraka Zako. Tunapofanya kazi zetu kama wahudumu, kuwaombea na kuwawekelea mikono, jalia, Bwana, ya kwamba wataponywa katika Jina la Mwanao, Bwana Yesu, Ambaye alisema, “Mwombeni Baba lo lote katika Jina Langu, nitalifanya.” Tungewezaje kulitilia shaka, kama Mungu alisema hivyo? Kama tu vile zile nabii za Danieli zilipaswa kutimizwa, kama vile kweli Mungu aishivyo, kila Neno halina budi kutimizwa. Nami naomba ya kwamba utatujalia kwa ajili ya utukufu Wake. Amina.

¹¹³ Ninaamini kwa unyenyekevu kabisa, na uaminifu na unyofu wa moyo wangu, ya kwamba kama wanaume kwa wanawake kule nje mlioinua mikono yenu kumkubali Bwana Yesu kama Mwokozi wenu binafsi...Najua ni kawaida kuwaleta watu kwenye madhabahu. Hiyo ni sawa. Sipingi jambo hilo. Bali kuja madhabahuni, unaweza tu kufanya jambo moja, na hilo ni, umwambie Mungu ya kwamba unashukuru alikuokoa. Kwa kuwa, mara unapomaanisha unalosema, unapoinua mikono yako, Mungu anakukubali kwa ushuhuda wako wakati huo. Uliasi kanuni za nguvu za uvutano, jinsi tu ile Nyota ilivyoasi kanuni za mfumo wa jua.

¹¹⁴ Mfumo wa jua husogea kulingana na utaratibu fulani. Hivyo ndivyo unavyopaswa kusogea. Bali Nyota hii iliasi huo, ikapita juu ya kila kitu, kwa maana Mungu ndiye aliyekuwa anaongoza.

¹¹⁵ Leo utaratibu wa kawaida unasema wengi wenu hapa hamna budi kufa. Daktari amefanya yote awezayo kufanya. Hiyo ni kweli. Bali Roho wa Mungu aliye hai aliasi hilo, kasema, "Nitawafanikisha." Haiwezi, huenda isitendeke katika sekunde moja. Walivumilia, kama kwamba wanamwona Yeye aliyekuwa haonekani. Ibrahimu alipewa ahadi, naye akangojea miaka ishirini na mitano kabla haijatendeka, bali alisonga mbele na kuita cho chote kilichokuwa dhidi ya ile ahadi kana kwamba hakikuwako.

¹¹⁶ Nisingeweza kusimama hapa katika mkesho huu wa Krismasi na kusema mambo haya mbele ya kudi hili dogo la watu kama sikujua nilichokuwa ninazungumzia.

¹¹⁷ Jana, huenda mwanamke huyo yuko hapa, jina lake ni Bibi Wright. Uko hapa, kutoka New Albany, Bibi Wright? Huenda wengi wenu mnamjua. Yeye, naamini, ni mwanamke anayejulikana sana na watu huko New Albany. Ile ibada ya mwisho ya kuponya hapa, ambapo...sikujua; ilikuwa katika upambanuzi. [Mahali patupu—Mh.]

¹¹⁸ Jumapili ijayo usiku, Bwana akipenda, huenda tukajaribu upambanuzi. Hatuwezi kufanya hilo Jumapili asubuhi, vizuri, kwa sababu mlima asubuhi ya Jumapili iliyopita, kama juma moja, yaliyotukia. Mnaona, watu hawafiki hapa kwa wakati mzuri kufanya mstari, na kadhalika, asubuhi, maana mna vyombo vyenu vya kuosha, na kadhalika. Lakini, Jumapili usiku, tutajaribu labda Jumapili usiku, Bwana akipenda.

¹¹⁹ Wakati upambanuzi ulikuwa ukiendelea, nataka tu kutaja kisa kimoja, mara baada ya kuwaambia juu ya Bibi Wright.

¹²⁰ Yeye hangaliweza kufika hapa. Madaktari wa New Albany, ningeweza kuyataja majina yao, bali huenda lisiwe jambo la hekima kufanya hivyo, maana mara nyingi hawataki hivyo, wewe kufanya hivyo. Tunajaribu kuishi kwa amani na watu wote, kama yamkini.

¹²¹ Nasi tunawapenda madaktari wetu. Madaktari, labda, wanaketi hapa asubuhi ya leo. Nina marafiki wengi madaktari, watu wazuri, Wakristo wanaomwamini Mungu. Wao si waponya; wao ni watu tu. Na wanaloweza kufanya, kimwili, wangefanya. Wao wanayasaidia tu maumbile. Wao hawa-... Wanaunga mfupa mahali pake; wanatoa kivimbe, kitu kama hicho. Bali Mungu hana budi kuumba chembechembe za mwili. Mungu ndiye tu anayeweza kuponya, ama—ama kufanyiza nyama; hakuna dawa inayoweza kufanya hivyo.

¹²² Sasa, mwanamke huyu alikuwa na mvilio wa damu kwenye moyo wake. Alikuwa na umri wa miaka sitini na kitu. Alikuwa amevimba sana hata akawa mnene tena kama alivyokuwa hapo awali. Nao wakapiga simu, naye mke wangu akaniitia hiyo simu, akasema, “Billy, wao... mwanamke fulani anataka kuzungumza nawe, huko New Albany.”

¹²³ Nikasema, “Vema, dada, njoo, asubuhi hii. Tutakuwa na ibada ya kuponya kwenye Maskani.”

¹²⁴ Akasema, “Ndugu yangu mpendwa,” akasema, “laiti ningalimleta, bali hata hawezi kusogea.” Kisha akasema, “Anakufa sasa hivi.” Akasema, “Hapana tumaini kwake.” Ndipo akasema, “Tumesikia mambo makuu ambayo Mungu amefanya kwa maombi yako. Mbona usimwombee? Je! utakuja?”

¹²⁵ Nikasema, “Siwezi kuja. Lakini unaweza kuweka simu sikioni mwake?”

¹²⁶ Akasema, “Naamini ninaweza kusogeza kitanda chake hapa.” Naye akasogeza kile kitanda pale, nikampata yule mwanamke; ilikuwa vigumu kwake kuzungumza.

¹²⁷ Nikasema, “Kama utaamini!” Imani ni bayana ya mambo yatarajiwayo. Si yale unayowazia tu; bali yale ujuayo kweli. Imani ni...

¹²⁸ Nilisema Jumapili ile nyingine, “Kama nilikuwa ninakufa kwa njaa, nami nikaomba...” Mkate mmoja utayaokoa maisha yangu, nawe unipe senti ishirini na tano; Ningefurahia tu kana kwamba nilikuwa na huo mkate, maana kuna mikate mingi.

¹²⁹ Basi kuna nguvu nyingi sana za kuponya. “Kama waweza kuamini,” hizo ndizo zile senti ishirini na tano; naweza kushangilia. Maana, labda mikate iko maili kumi kutoka nilipo mimi, lakini, ninapokuwa na hizo senti ishirini na tano, imani ni bayana ya mambo yatarajiwayo. Ninafurahia tu zile senti ishirini na tano kama kwamba nilikuwa ninakula huo mkate, ingawa bado ningali nina safari ndefu; nivuke kingo za kijito, na kuvuka vivuko, na kuruka visiki, na kushuka kwenda nikipita njia zenye miiba, na kupanda kilima. Huenda nikazidi kupata njaa wakati wote, hata nipindwe na misuli; nina njaa kwelikweli. Bali nitashangilia wakati wote, kwa maana nimeshikilia zile senti ishirini na tano, zinazotosha kununulia huo mkate, hata hali za mambo ziweje.

¹³⁰ Ibrahimu alifurahi kwa miaka ishirini na mitano, akishikilia imani moyoni mwake ya kwamba Mungu aliweza kutekeleza yale aliyoahidi. Naye akapata alichoomba.

¹³¹ Dada mpendwa, pale. Haidhuru hali ya mambo iweje, chukua hizo senti ishirini na tano, hiyo imani, i-m-a-n-i. Ishike kwa mkono, iweke moyoni mwako, useme, “Hata iweje . . .” Sasa huwezi kujifanya unaamini. Huna budi kuamini kweli. “Mtoto wangu ataishi, kwa maana moyoni mwangu . . . Mungu ametoa ahadi, nami nina imani ya kuamini jambo hilo.” Ndipo mengine yote yanakuwa kinyume. Mnaona? Mungu huifanya iingie mle ndani katika—katika kiwango kile.

¹³² Mwanamke huyo alinipigia simu jana. Wengine wao walijibu hiyo simu; hangekubali kuzungumza. Mke wangu akaenda kuichukua simu; hangekubali kuzungumza. Yeye alitaka kuzungumza nami. Akasema, “Ndugu Branham, ninalisifu jina lako.”

Nikasema, “Ati jina langu? Unafanya hivyo kwa madhumuni gani?”

Akasema, “Loo, laiti ungaliniona!”

Nikasema, “Basi msifu Mungu, Ndiye aliyefanya hivyo.”

¹³³ Akasema, “Kule wale madaktari hata hawawezi kupata kule kuvilia damu. Kumetawanyika na kutoweka. Nami ni mzima, nikitembea kila mahali na afya nzuri, afya nzuri sana niliyowahi kupata katika miaka kadha.” Jina lake ni Bibi Wright. Anaishi sasa . . . Yeye aliniambia jina lake la kwanza. Mahali fulani huko New Albany, sijui sasa hivi.

¹³⁴ Katika upambanuzi, Jumapili iliyopita, ilikuwa juma moja, nikisimama hapa. Nikasema, “Sitaki mtu ye yote wa hapa Maskanini. Nataka wale wasio wa haya Maskani. Roho Mtakatifu na anene.” Lakini kwa namna fulani, huko nyuma mahali fulani upande mmoja ama mwingine, kulikuwa na jamaa mdogo jina lake Hickerson, sisi sote tunamjua Ndugu Hickerson. Yeye ni kumbukumbu halisi sana la neema ya Mungu. Basi alikimbia chini ya watu fulani. Hata sikumjua. Bali Roho Mtakatifu tayari alikuwa ameyaamuru yote. Alikuwa akiangalia kupitia mkono wa mtu fulani, akiketi kule nyuma, nami sijui alikuwa nani.

¹³⁵ Nami nikasema, “Yule jamaa mdogo anayeniangalia, kupitia kwenye mkono wa mtu yule. Yeye anamwombea mpendwa wake, naamini, nduguye ama shemejiye, ama ye yote yule, aliyekuwa kwenye hospitali ya wenda wazimu; amerukwa na akili, na hakuna tumaini kwamba atapona.” Nayo ikasema, “BWANA ASEMA HIVI. Yeye atapata afya.” Na maskini jamaa huyo akaamini, ingawaje sikujua habari zake kwa siku kadha baadaye.

¹³⁶ Basi jana walimtoa kwenye hospitali ya wenda wazimu huko Kentucky, akiwa, “mtu mwenye akili timamu kabisa, amekuwa mzima.” Na maskini ndugu yetu mhubiri wa Kimethodisti, Ndugu Collins, kumbukumbu nyingine ya neema ya Mungu. Huenda akawa hapa asubuhi ya leo. Wote wawili, wote, huenda wakawa hapa. Walikuja nyumbani kwangu jana usiku, pamoja na Ndugu Palmer kutoka Georgia, na walikuwa wakiniambia ya kwamba mvulana huyu alipita hapa, akienda zake Louisville, baada ya kuruhusiwa atoke katika hospitali ya wenda wazimu. Ameokoka, pia, naye alikuwa anashuka kwenda kutengeza mambo yote aliyokuwa amefanya; kumbukumbu. Neema ya Mungu idumuyo!

¹³⁷ Ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Usimruhusu adui akudanganye. Kuna Mwangi usiozimika unaoangaza; huo Mwangi usiozimika ni Yesu Kristo, Mwana wa Mungu. Mwamini Yeye. Itie nanga moyoni mwako. Ipokee kama imani.

¹³⁸ Na tuombeni na tujue, tuwawekee mikono, tukiwapaka mafuta, muone atakavyofanya Mungu, hata hali ya mambo iweje.

¹³⁹ Yesu alisema, katika Marko 11:24. Yeye alisema, “Ukiuambia mlima huu, ‘Ngo’ka ukatupwe baharini,’ na usione shaka moyoni mwako, ila uamini kwamba hayo uliyosema yatatukia, yatakuwa yako.”

¹⁴⁰ Sasa hebu niinukuu kamusi, hiyo ni ya Kiyunani asili. Hivi ndivyo inavyosema. “Kama utauambia mlima huu, ‘Inuliwa juu ukatupwe baharini,’ na usione shaka moyoni mwako, ila uamini ya kwamba yale umesema yatatukia, yatakuwa yako.”

¹⁴¹ Uliposema, “Mlima, ng’oka,” na ungali umesimama pale, unasema, “Vema, haikutukia”? Loo, kweli ilitendeka. Uliposema, “Ewe mlima, ng’oka,” labda chembe moja ya mchanga isiyo na maana iliachilia, toka kwa mamia ya mabilioni na mabilioni ya tani. Chembe moja ndogo ilisogea, lakini limeanza kutukia. Shikilia imani hiyo na uangalie huo mlima ukitoweka. Hakika.

¹⁴² Utasema moyoni mwako, “Ewe ugonjwa, ondoka kwa mtoto wangu. Ewe ugonjwa, toka katika mwili wangu, katika Jina la Bwana Yesu,” na usione shaka. Papo hapo zile chembechembe zenye afya zinatwaa silaha na zana mpya za vita, na adui anaanza kurudi nyuma. Yeye ameshindwa kwa sababu Kristo, katika kunywa manemane Yake pale Kalvari, alimshinda Ibilisi na kila moja ya nguvu zake. Kisha akamvua kila kitu alichokuwa nacho, naye si kitu ila ni laghai tu; anaweza kumaliza nayo, atafanya hivyo.

¹⁴³ Sisi tumeazimia, kwa neema ya Mungu, kuihubiri Injili na kurudisha mng’ao wa Mwangi Wake hata atakapokuja.

¹⁴⁴ Sasa, Bwana, yaliyoisalia ni Yako. Sasa tutawaita watu hawa, na jalia Roho Mtakatifu aje katika Maskani haya madogo

na afanye imani katika kila moyo, wanaposimama na kupitia hapa wapate kuombewa. Jalia waondoke leo na wafanye kama wale mamajusi; walipoiona ile Nyota tena, baada ya kipindi cha giza, walishangilia kwa furaha kubwa mno; basi jalia watu hawa, wanapopakwa mafuta na kuombewa, Yakobo alisema, katika Injili, "Waite wazee wakawapake mafuta na kuwaombea. Kule kuomba kwa imani kutamwokoa mgonjwa yule." Jalia hawa watu washangilie kwa furaha kubwa mno, wakijua ya kwamba imani ya Mungu imepenya ikaingia mioyoni mwao, nao watapata wanayoomba.

¹⁴⁵ Sasa, Baba, Wewe umetenda sehemu Yako. Mimi nimetenda yote nijuayo jinsi ya kufanya, isipokuwa kuwawekelea watu mikono na kuwapaka mafuta. Sasa mengine yatakuwa yao. Naomba lisishindwe. Jalia kwamba kila gurudumu la saa idumuyo ya Mungu lifanye kazi kikamilifu asubuhi hii, wagonjwa wanapopakwa mafuta. Tunaomba kwa ajili ya Yesu Kristo, katika Jina Lake. Amina.

Kama tu waweza kuamini, amini tu,
Yote yatendeka, amini . . .

¹⁴⁶ Jinsi wimbo huo unavyofanya jambo fulani kwangu! Lugha mia kadha . . . Nimewasikia makafiri na Wahotentoti wakiuimba huo nilipokuwa nikija jukwaani.

¹⁴⁷ Mwanamke yuyu huyu, piano ii hii, kadiri nijuavyo mimi, alinijulisha huo wimbo, miaka kumi na mmoja iliyopita, kabla sijaondoka hudumani. Paul Rader, rafiki yangu, alivandika.

¹⁴⁸ Yesu, akishuka toka mlimani, alimwona mvulana mwenye kifafa. Wanafunzi hawakuweza kufanya kitu juu yake. Yeye akasema, "Bwana, mrehemu mtoto wangu."

¹⁴⁹ Yeye akasema, "Naweza kama utaamini, kwa maana mambo yote yanawezekana; amini tu." Hapo ndipo Paul alipopata fungu lake la maneno, *Amini Tu*. "A- . . ."

¹⁵⁰ Sasa usivangalie ugonjwa wako sasa. "Ami- . . ." Je! huwezi kufanya hivyo? "Mambo yote yanawezekana, tu. . ."

¹⁵¹ Kumbukeni tu, Yeye anasimama hapa. Yeye ni mwema sana. Ameahidi jambo hilo. Yeye hurudisha mng'ao wa miangaza Yake; angalia wengine wakiponywa. Bila shaka, waweza, pia. "Nitazame mimi," kipofu aliyeponywa, unaona. Waangalie wengine, angalia jinsi, jamani, yale Bwana ametenda! ". . . yawezekana. . ."

¹⁵² Wangapi wanaamini sasa hivi ya kwamba mna imani mioyoni mwenu ya kusema, "Naamini imekwisha. Naamini naweza kumpokea sasa hivi. Naamini naweza kusema ya kwamba nitapata afya. Haidhuru nini kimetendeka, ninauambia huu mlima wa maradhi, 'Ng'oka ukaniache, ama wapendwa wangu, ama cho chote kile. Nami naamini yatatukia."?

153 Angalia yatakayotukia. Huo ugonjwa utaanza kupasuka. Utaanza kuondoka. Muda si muda, daktari atasema, “Imekuwaje hapa?” Hiyo ni kweli, kama waweza kuamini.

154 Waweza kuja, Ndugu Neville? Naam, hebu wale walio kwenye haya marefu ya kanisa *hapa*, wasimame upande *huu*. Nanyi mlio kwenye marefu *haya*, zungukeni huko nyuma hata mje upande huu, tafadhalini, kusudi tuwe na mstari mmoja pekee. Tungetaka wazee waje huku mbele, wasimame pamoja na watu, wanapoombewa.

155 Sasa, yule msichana mdogo, tutashuka twende tukamwombee huyu mtoto mchanga aliyelala hapa. Tutakuja tu moja kwa moja pale alipo.

156 Nataka wale ambao... wengine watakaombewa, waende upande huu sasa. Nataka kila mtu humu ndani awe katika maombi sasa hivi. Una sehemu katika jambo hili. Hao mabawabu wanaosimama pale watakuelekeza kwenye mstari unaopaswa kufanya wakati huu.

Yote yatendeka, amini tu.

Msiogope, enyi kundi dogo, tangu kwenye ule msalaba hadi kwenye kiti cha enzi;

Tangu mauti hadi uzimani Yeye alienda kwa ajili ya walio Wake;

Katika nguvu duniani, nguvu zote kule juu, Amepewa Yeye kwa ajili ya kondoo wa upendo Wake.

Sasa nyota ya Krismasi inasema nini?

Amini tu, amini tu,
Yote yatendeka, amini tu;
Amini tu, amini tu,
Yote yatendeka, amini tu.

157 Marafiki wangu wapendwa, kuna wengi humu ndani wanaowaombea sasa; wanaume wazuri na wanawake wazuri, watakatifu, wanaume na wanawake wacha Mungu.

158 Ndugu yangu Neville anasimama hapa karibu nami, ambaye nimemjua kwa miaka mingi kuwa mcha Mungu. Watu wanaokuja hapa kutoka nje ya mji, walini pigia simu, wakasema, “Huyo jamaa mdogo aliye mchungaji wenu ni nani? Nipe anwani yake; nataka kumwandikia. Anaonekana kama mtu mwaminifu sana.” Mimi nina furaha sana ya kwamba naweza kusema, “na ni mmoja wa watu wacha Mungu sana niwajuao.” Yeye anaishi anayohubiri na kuzungumzia. Yuna chupa ya kupakia mafuta mkononi mwake.

Mungu ndiye aliye na nguvu mkononi Mwake.

159 Je, una imani moyoni mwako? Kama unayo, haina budi kutukia. Kule kupitia hapa, hapa kuna wahudumu, watu wacha

Mungu wanaoketi hapa watakuwa wakiwaombea. Kitu fulani hakina budi kutendeka sasa.

¹⁶⁰ Kitu fulani kilikuleta umbali huu; ilikuwa ni ile Nyota, sasa, ile Nyota, Nyota ya Asubuhi. Sasa pokea Mwanga usiozimika na wa Milele. Kama tu vile ninyi, tunafuata taratibu hii, kama vile kuwabatiza, ama cho chote kile, mnaona. “Wapakeni mafuta walio wagonjwa, waombeeni; kuomba kwa imani kutawaokoa walio wagonjwa.”

¹⁶¹ Yesu alisema, maneno ya mwisho kwa Kanisa Lake. “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio; wataweka mikono yao juu ya wagonjwa, nao watapata afya.” Kwa maneno mengine, ningetaka kusema jambo hili, kuyaweka katika maneno mpate kufahamu, “Po pote Injili hii itakapohubiriwa, ulimwenguni kote, watumishi Wangu watawawekea mikono walio wagonjwa, watapata afya.” Sawa. Mnaona?

¹⁶² Sasa kuna jambo moja tu la kuhukumu hilo, hilo ni, kutokuamini. Mnaona, hilo halitegemei...hata kama—kama ndugu fulani pamoja nami tulikuwa...hatukustahili hata kuihubiri Injili; ambayo, hatustahili, ila kwa neema Yake tu. Lakini, hata tuwe nini, ni Neno Lake. Yeye, si lazima aambatane nasi, bali hana budi kudumu na Neno Lake, “Kama waweza kuamini.”

¹⁶³ Basi wangapi huko kwenye kusanyiko watakuwa wakiwaombea watu hawa? Inueni mikono yenu. Sasa nawatakeni ninyi watu mwangalie kule. Huko ndiko maombi yanakoenda, kuelekea Mbinguni kwa ajili yenu sasa. Sasa huku kila kichwa kimeinamishwa na kila mmoja akiomba, huku ndugu anawapaka mafuta.

¹⁶⁴ Hebu kidogo sasa, tutafanya maombi haya ya kusanyiko kwa ajili ya hawa hapa.

¹⁶⁵ Bwana mwenye rehema, tunasonga mbele sasa kama watumishi Wako, kufanya wajibu wa wahudumu. Kuna wengi hapa, Bwana, mstarini, ambao ni wagonjwa sana, sana, hapana shaka. Wengine wao ni mahututi kabisa. Na wengine wao wangali kwenye viti vyao. Kwa mafano, yule msichana mdogo aliyetoka Florida. Kuna wengine hapa wametoka Georgia na kutoka mahali mbalimbali, kutoka huko Indianapolis, wengine kutoka huko Ohio, wamekusanyika katika kundi hili dogo asubuhi ya leo, wamekuwa wakingojea hapa katika mahoteli na kila kitu, wakingojea saa watakayoombewa. Wamekuwa katika mikutano hii. Wameangalia mkono Wako ukitembea na kutenda kazi. Na papa hapa sasa ile...Bwana, ondolea mbali ile hadithi ya uongo ya Baba Krismasi uwalettee zawadi iliyo halisi ya Krismasi. Wape afya njema sasa hivi, Bwana, kwa maana wao wamekuja wakiamini.

¹⁶⁶ Nasi tunakuja, tukisimama kati yao na Bwana Mungu wa Mbinguni, kuwaombea, kuomba dua na kusema kwa sauti zetu

wenyewe, kwa niaba yao. Jalia hata mmoja wao, Bwana, asikose kuwa na imani.

¹⁶⁷ Tunajua Neno linasema jambo hilo. Tunajua ya kwamba tunaliamini. Sasa, Bwana, naomba kwamba waliamini na wapokee walichoomba. Tunasonga mbele sasa kama wajumbe wa Kristo, pamoja na kundi hili lote la kanisa, tukiomba kwa moyo mmoja kwa ajili ya kuponywa kwao. Na iwe hivyo. Na wakati waondokapo, na waende na furaha kubwa mno kwa sababu Ma—Mapambazuko yametufikia. Miangaza mikuu ya Mbinguni imeelekea kwetu, na tunamwona Bwana Yesu aliyefufuka katika Nguvu na Utukufu Wake. Amina.

¹⁶⁸ Wakati anapopakwa mafuta, katika Jina la Bwana Yesu, tunaweka mikono yetu juu yake, na kuomba ya kwamba ugonjwa wake uponywe na mkono wa Mwenyezi Mungu, katika Jina la Yesu. Amina.

¹⁶⁹ Mungu akubariki. Nenda ukapokee, katika Jina la Bwana Yesu.

¹⁷⁰ Wakati anapopakwa mafuta, katika Jina la Bwana Yesu, tunaomba kwamba haja ya moyo wake ijaliwe, katika Jina la Bwana Yesu.

¹⁷¹ Anapopakwa mafuta, tunamwekelea mikono ndugu yetu, katika Jina . . .



MWANGA MKUU UNAONG'AA SWA57-1222
(The Great Shining Light)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumapili, tarehe 22 Desemba, 1957 katika Maskani ya Branham kule Jeffersonville, Indiana, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©1992 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org